

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA YA MATANGAZO YA FAINI YA UKIUKWAJI WA KANUNI ZA MAKOSA YA JINAI (CCIN)

Nini maana ya CCIN?

CCIN ni Tangazo la Faini ya Ukiukwaji wa Kanuni ya Kosa la Jinai ambalo linatolewa kwa wakosaji wa makosa ya jinai madogo.

Ni Makosa gani?

Kanuni ya Jinai s378 Kuiba pale ambapo thamani ya vitu vilivyoibiwa ni chini ya \$500.00

Kanuni ya Jinai s74A (2) Tabia mbaya

Nitatakiwa kulipa ngapi?

Adhabu iliyopitishwa ya makosa ya CCIN ni \$500.00.

Adhabu iliyopitishwa ni ipi?

Adhabu iliyopitishwa ni kiasi kinachotakiwa kwa mtu anayedaiwa kukosa lazima kulipa kama anataka jambo kushughulikiwa nje ya Mahakama. Adhabu iliyopitishwa ni chini ya adhabu iliyowekwa kwa ajili ya kosa hilo.

Natakiwa kuwa na umri wa kiasi gani ili kupata CCIN?

CCIN inaweza kutolewa kwa mkosaji mwenye miaka 17 au zaidi.

Kwa nini Polisi wa Australia ya Magharibi wanatoa CCIN?

Sheria chini ya *Kanuni ya Jinai ya Marekebisho (sheria ukiukwaji)* Sheria ya 2011 sasa itawezesha Polisi wa Australia Magharibi (WA Police) kutoa faini ya ukiukwaji kama chaguo mbadala ya kukabiliana na makosa ya jinai ya Maadili na Polisi wa WA lazima kutekeleza sheria hiyo. Zamani polisi walikuwa wakichukua wahalifu kituo cha polisi ili kushtakiwa. Utaratibu huu unaondoa polisi kutoka katika mitaa. Kutoa CCIN kutaruhusu maafisa wa polisi kubaki katika mitaa kulinda jamii na kupunguza idadi ya makosa madogo madogo kuwakilishwa mahakamani.

Inatokea nini kama nikipewa CCIN?

Afisa wa uchunguzi ataongea na wewe kuhusu tukio na kuchukua maelezo yako. Alama za vidole vyako na picha (na uwezekano wa DNA yako) vinaweza kuchukuliwa wakati huo huo. Kama unastahili utaambiwa kama CCIN itatolewa kwako.

Hili ni kosa langu la kwanza - je nitapata rekodi ya uhalifu kama matokeo ya hii CCIN?

Kama hili ni kosa lako la kwanza na kosa la ukiukwaji limelipwa lote hakuna hatia ya makosa ya jinai yatayowekewa kumbukumbu.

Inatokea nini kama nina rekodi ya awali kwa ajili ya makosa yanayofaa?

Utoaji wa CCIN si lazima na afisa wa uchunguzi atatumia busara zake kama njia ya sahihi ya utekelezaji kwa ajili ya tukio hilo, ambayo inaweza kuhusisha kuonekana Mahakama. Kama afisa akiamua kwamba kutoa CCIN ni sahihi, na kama ukiukwaji ni kulipwa hera yote, hakuna hatia ya makosa ya jinai yatawekwa kumbukumbu kwa kosa hili husika.

Ninalipa namna gani kama nikipewa CCIN?

Njia za malipo zimeorodheshwa katika sheria ya makosa ikiwa ni pamoja;

- Kulipa mwenyewe kwenye posta ya Australia
- Kwenye mtandao
- Kwa posta
- Kwa simu

Itatokea nini kama sitalipa faini kwa mda niliopewa ?

Kama malipo yote hayajapokelewa katika siku 28, barua ya Mwisho ya kutakiwa kulipa itatumwa kwako na gharama zilizoongezwa. Ombi la Mwisho la Kutakiwa kulipa lazima kulipwa ndani ya siku 28 ya suala tarehe iliyoko kwenye taarifa hiyo.

Kama malipo hayajapokelewa tarehe ilivyoainishwa kwenye taarifa ya Mwisho ya Kulipa, ukiukwaji utasajiliwa katika Faini ya Utekelezaji wa Msajili, ambayo hubeba gharama zaidi na inawezekana kusimamishwa gari yako na / au leseni ya udereva.

Maelezo yako pia yanaweza kuchapishwa kwenye tovuti; gari yako inaweza kusimamishwa au kuondolewa namba za sahani yako ya gari, na mali yako inaweza kuchukuliwa na kuuzwa.

Ni gharama zipi za ziada?

Ada ya ziada inahusiana na gharama za utendaji na posta kwa ajili ya taarifa ya mwisho ya kulipia na kwa sasa ni \$ 14.65. Gharama zaidi zitatozwa na Msajiri wa Utekelezaji wa Faini.

Je naweza kufanya malipo nusu?

Hapana, sheria inaonyesha kuwa malipo lazima yalipwe yote kabla ya tarehe iliyoandikwa.

Je naweza kuomba kurudiwa kwa CCIN?

Ndiyo, kurudiwa kwa faini ya ukiukwaji inaweza kupatikana kwa kuomba kwa maandishi kwa Mhusika wa Ukiukwaji * Uendeshaji, rejea kwenye anwani iliyoko nyuma inayohusiana na tangazo au barua ya Ukiukwaji.

Je naweza kuchagua kwenda mahakamani na inatokea nini kama nikichagua hivyo?

Ndiyo, unaweza kuchagua kwenda Mahakama. Ni lazima kujaza fomu ya Kipengere cha Kuteua kifungu cha Mahakama chaa Ilani ya ukiukwaji na baada yake unatakiwa kutuma kwa Mhusika wa Ukiukwaji * Kitengi wa Uendeshaji katika anwani zilizomo katika fomu. Kama ukipatikana na hatia ya kosa utapata rekodi ya uhalifu kwa kosa fulani.

Alama za vidole vyangu na/au DNA vilichukuliwa - nini kinachotokea?

Mara baada ya faini ya ukiukwaji imeweza kulipwa kikamilifu unaweza kuandika kwa Kamishna wa Polisi na kuomba kwamba alama za vidole yako na au DNA zinazohusiana na tukio la CCIN ziondolewe kutoka kumbukumbu za Polisi ya WA

Je naweza kuomba Ushauri wa Kisheria?

Ndiyo.